



Angalizo: Ndoto inaweza kuwa na tafsiri zaidi ya moja, hivyo baada ya kusoma tafsiri hizi, ni vyema ukaketi na kumwuliza Roho Mtakatifu kwa uthibitisho kamili.

---

Kibiblia Ng'ombe anawakilisha "Mwaka". Kama kabla ya kulala ulikuwa huwazi mambo ya Ng'ombe wala kuyatafakari kwa siku hiyo, halafu ukajikuta usiku au mchana umeota Ng'ombe, aidha anakukimbiza, au wewe unamchunga, basi ifuatayo inaweza kuwa tafsiri yake.

Ng'ombe kibiblia anawakilisha "Mwaka"... akiwa mmoja ni mwaka mmoja, wakiwa wawili ni miaka miwili,...wakiwa saba ni miaka saba n.k

Mwanzo 41:26 "Wale ng'ombe saba wema ni miaka saba; na yale masuke saba mema ni miaka saba. Ndoto ni moja.

27 Na wale ng'ombe saba, dhaifu, wabaya, waliopanda baada yao, ni miaka saba; na yale masuke saba matupu yaliyokaushwa na upemo wa mashariki, yatakuwa miaka saba ya njaa".

Kwahiyoo ukiona Ng'ombe anakufukuza basi huenda huo mwaka uliopo, unamisuko suko mingi, au utakuwa na misukosuko mingi..Suluhisho ni kumkaribia Mungu Zaidi na kuomba..

Vile vile ukiona umempanda Ng'ombe na anakimbia sana kwa hatari basi vile vile huo mwaka utakubeba lakini utakuwa na hatari nydingi..

Ukiona unamchunga Ng'ombe vizuri na anatoa maziwa mengi, basi mwaka utakuwa wa neema, au kuna neema ikiwa utadumu katika Imani.

Mbali na hayo, Ng'ombe pia anaweza kuwakilisha roho za mapepo, kutegemea ndoto uliyoota. Kama hujampokea Yesu na umeota Ng'ombe anakufukuza nawe unakimbia sana



Kuota Ng'ombe (Unakimbizwa, umempanda n.k)

kwa hofu, huwenda pia upo mikononi mwa ibilisi, na anakuonea katika ulimwengu wa roho.

Hivyo suluhisho ni kutubu na kumkaribisha Bwana YESU maishani mwako.

KUOTA UMEKUFA

KUOTA MOTO UMEWAKA

KUOTA UPO JANGWANI PEKE YAKO

KUOTA UNAKIMBIZWA NA SIMBA

KUOTA MTI UMEANGUKA